

KUMB: PPR/15 - 05/1

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA
JUMATANO, TAREHE 6 Mei 2015**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 6 Mei 2015**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote yaani Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 1 Aprili 2015. Kwa Mwezi Mei 2015, bei za rejareja kwa Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa Sh 111/lita sawa na asilimia 6.32% na Sh 23/lita sawa na asilimia 1.37%, sawia, ambapo bei ya rejareja ya Mafuta ya Taa imeshuka kwa Sh 31/lita, sawa na asilimia 1.86%. Kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita bei za jumla kwa mafuta ya Petroli na Dizeli pia zimeongezeka kwa, Sh 110.85/lita sawa na asilimia 6.72% ,Sh 22.94/lita sawa na asilimia 1.46% sawia, na Mafuta ya Taa imeshuka kwa Sh 30.70/lita sawa na asilimia 1.98%. Mabadiliko haya yametokana na mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la dunia na kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani.
- (b) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2008, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (c) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani ilimradi bei hizo ziko chini ya bei kikomo (price cap) kama ilivyokokotolewa na fomula iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 7 la tarehe 4 Machi 2015.**
- (d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionyesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta kutoka kwenye vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja na adhabu itatolewa kwa kituo husika.**
- (e) Wanunuzi wanashauriwa kuhakikisha kuwa wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo; ama endapo utakuwa umeuziwa mafuta yenye kiwango cha ubora kisichofaa.

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Sh/Lita)	Dizeli (Sh/lita)	Mafuta Ya Taa (Sh/Lita)
Dar es Salaam	1,866	1,695	1,624
Arusha	1,950	1,779	1,708
Arumeru (Usa West)	1,950	1,779	1,708
Karatu	1,968	1,797	1,726
Monduli	1,955	1,784	1,713
Ngorongoro (Loliondo)	2,006	1,835	1,764
Kibaha	1,871	1,699	1,628
Bagamoyo	1,877	1,706	1,635
Kisarawe	1,873	1,702	1,631
Mkuranga	1,876	1,704	1,634
Rufiji	1,894	1,722	1,651
Dodoma	1,925	1,753	1,682
Bahi	1,932	1,761	1,690
Chemba	1,951	1,780	1,709
Kondoa	1,957	1,786	1,715
Kongwa	1,922	1,750	1,680
Mpwapwa	1,926	1,754	1,684
Iringa	1,930	1,759	1,688
Kilolo	1,934	1,763	1,692
Mufindi (Mafinga)	1,940	1,769	1,698
Njombe	1,958	1,787	1,716
Ludewa	1,996	1,825	1,754
Makete	1,989	1,818	1,747
Wanging'ombe (Igwachanya)	1,956	1,785	1,714
Bukoba	2,081	1,910	1,839
Biharamulo	2,055	1,884	1,813
Karagwe (Kayanga)	2,097	1,926	1,855
Kyerwa (Ruberwa)	2,103	1,932	1,861
Muleba	2,081	1,910	1,839
Ngara	2,046	1,875	1,804
Misenyi	2,089	1,918	1,847
Geita	2,031	1,860	1,789
Bukombe	2,020	1,849	1,778
Chato	2,052	1,881	1,810
Mbogwe	2,069	1,898	1,827

Nyang'hwale	2,046	1,875	1,804
Kigoma	2,097	1,925	1,855
Uvinza (Lugufu)	2,109	1,938	1,867
Buhigwe	2,086	1,915	1,844
Kakonko	2,054	1,883	1,812
Kasulu	2,083	1,911	1,841
Kibondo	2,061	1,890	1,819
Moshi	1,940	1,768	1,697
Hai (Bomang'ombe)	1,943	1,771	1,701
Mwanga	1,933	1,761	1,691
Rombo (Mkuu)	1,961	1,789	1,718
Same	1,926	1,755	1,684
Siha (Sanya Juu)	1,946	1,775	1,704
Lindi	1,925	1,753	1,683
Kilwa Masoko	1,900	1,728	1,658
Liwale	1,946	1,774	1,704
Nachingwea	1,954	1,782	1,712
Ruangwa	1,952	1,781	1,710
Babati	1,988	1,817	1,746
Hanang (Katesh)	1,999	1,827	1,756
Kiteto (Kibaya)	1,999	1,828	1,757
Mbulu	2,001	1,829	1,759
Simanjiro (Orkasumet)	2,020	1,849	1,778
Musoma	2,044	1,873	1,802
Rorya (Ingirijuu)	2,053	1,882	1,811
Bunda	2,035	1,864	1,793
Butiama	2,041	1,870	1,799
Serengeti (Mugumu)	2,090	1,918	1,848
Tarime	2,055	1,884	1,813
Mbeya	1,973	1,801	1,731
Chunya	1,982	1,811	1,740
Ileje	1,986	1,815	1,744
Kyela	1,989	1,817	1,746
Mbarali (Rujewa)	1,957	1,786	1,715
Mbozi (Vwawa)	1,982	1,811	1,740
Momba (Chitete)	1,991	1,820	1,749
Rungwe (Tukuyu)	1,982	1,810	1,740
Morogoro	1,891	1,720	1,649
Mikumi	1,907	1,735	1,664
Kilombero (Ifakara)	1,929	1,757	1,687
Ulanga (Mahenge)	1,939	1,768	1,697

Kilosa	1,909	1,738	1,667
Gairo	1,909	1,738	1,667
Mvomero (Wami Sokoine)	1,901	1,730	1,659
Turian	1,916	1,745	1,674
Mtwara	1,938	1,767	1,696
Nanyumbu (Mangaka)	1,987	1,816	1,745
Masaki	1,964	1,792	1,722
Newala	1,970	1,799	1,728
Tandahimba	1,963	1,792	1,721
Mwanza	2,016	1,844	1,774
Kwimba	2,052	1,880	1,810
Magu	2,024	1,852	1,782
Misungwi	2,021	1,850	1,779
Sengerema	2,048	1,877	1,806
Ukerewe	2,075	1,904	1,833
Sumbawanga	2,039	1,867	1,796
Kalambo (Matai)	2,031	1,860	1,789
Nkasi (Namanyeke)	2,052	1,881	1,810
Katavi (Mpanda)	2,074	1,902	1,831
Mlele (Inyonga)	2,052	1,880	1,810
Songea	1,989	1,818	1,747
Mbinga	2,023	1,851	1,780
Namtumbo	2,018	1,847	1,776
Nyasa (Mbamba Bay)	2,025	1,854	1,783
Tunduru	2,048	1,877	1,806
Shinyanga	1,995	1,823	1,752
Kahama	2,008	1,837	1,766
Kishapu	2,023	1,852	1,781
Simiyu (Bariadi)	2,036	1,865	1,794
Busega (Nyashimo)	2,029	1,858	1,787
Itilima (Lagangabilili)	2,039	1,868	1,797
Maswa	2,027	1,856	1,785
Meatu (Mwanhuzi)	2,035	1,863	1,792
Singida	1,957	1,785	1,714
Iramba	1,969	1,797	1,726
Manyoni	1,941	1,770	1,699
Ikungi	1,952	1,781	1,710
Mkalama (Nduguti)	1,981	1,810	1,739
Tabora	2,020	1,848	1,778
Igunga	1,974	1,802	1,732
Kaliua	2,038	1,867	1,796

Ulyankulu	2,032	1,861	1,790
Nzega	1,984	1,813	1,742
Sikonge	2,032	1,860	1,789
Urambo	2,033	1,862	1,791
Tanga	1,912	1,741	1,670
Handeni	1,892	1,720	1,649
Kilindi	1,926	1,755	1,684
Korogwe	1,905	1,734	1,663
Lushoto	1,915	1,743	1,673
Mkinga (Maramba)	1,926	1,755	1,684
Muheza	1,912	1,741	1,670
Pangani	1,919	1,747	1,677

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli (Sh/L)	Dizeli (Sh/L)	Mafuta ya Taa (Sh/L)
Bei Kikomo	1,761.05	1,589.58	1,518.86

Felix Ngamlagosi
MKURUGENZI MKUU
EWURA